
# NGURUMO ya MWANDISHI



Dawati la Mhariri: 0766-974 865

# TUSHIKANE MKONO

**Nakusalimuni kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ….**

Tumeuanza mwaka 2022 vizuri na tunamshukuru Mungu kwa kutupa nafasi nyingine ya uhai. Si kwa sababu tu wema sana, la! Bali kuna jambo lake ambalo hatujalikamilisha katika maisha yetu.

Kama tunavyojua kuwa kila mwaka mpya kuna tathmini ambayo yatupasa kufanya tukirejelea mipango tuliyojiwekea katika mwaka uliyopita. Je tumefanikiwa kwa asilimia ngapi? Au tumeshindwa kwa kiwango gani? Pale tuliposhindwa yatupasa kutafakari kwa nini nimeshindwa ili wakati mwingine tusirudie makosa yale yale.
Mwaka 2021 nilipata nafasi ya kukutana na waandishi kadhaa ambao wanachipukia katika tasnia hii. Pia nimesoma maandiko mengi ya wale ambao ningewaita chipukizi kama mimi. Katika mazungumzo nao wengi sana walilalamika jambo moja tu kuwa, waandishi wakubwa hawana msaada na sisi. Hivi ni kweli? Sina haja ya kuhoji sana ila nitasema kitu.

Sanaa ya uandishi wa vitabu inakuwa kwa kasi sana nchini Tanzania. Tumeshuhudia vitabu vikichapwa na wengine wakiweka mitandaoni kazi zao. Lakini ukizisoma utagundua kwamba hawa watu wana kitu kinachotakiwa kuibuliwa au kupaliliwa. Lakini nani mwenye kazi hiyo? Mawazo yangu ni kwamba mwaka huu wa 2022 itapendeza ukiwa mwaka wa kushikana mkono. Wale waandishi ambao tayari wamepiga hatua kubwa katika uga huu kuweza kuwasaidia hawa wanaochipukia kwa kuandaa warsha, semina au hata makongamano yatakayokuwa sehemu ya mafunzo ya uandishi wenye dira. ***R.M***

## Mariam Mbano; Mwaka 2022 Nitatoa kitabu (INSHAAALAH)



**Mwaka 2019 niliandika kitabu nikawaza ningetoa 2019 nikaghairi, mwaka 2020 nikakiongezea nikasema nitakitoa 2020 nikaghairi, mwaka 2021 nikakipitia tena nikataka nikitoe nikaghairi.**
Natumaini mwaka 2022 nitatoa kitabu changu cha kwanza Mwenyezimungu akipenda.

Kitabu kimeandikwa na Mariam Mbano
Kimepitiwa na Mohammed Hammie Rajab na Joylynn Manyaki
Kimehaririwa na Luqman Maloto
Kimehakikiwa na Bw. Ambrose Mghanga

Mmoja wa watu waliopata nafasi ya kukipitia ameseema kwamba;
Kitabu hiki kinafundisha vitu vingi kuhusu uhusiano. Nina uhakika ukimaliza kukisoma utakuwa mpya.
Kati ya mambo mengi, pia kinafundisha na kusaidia yafuatayo;


- Jinsi ya kupona machungu ya kuachana na namna ya kuvuka kipindi kigumu cha utengano.
- Kujijua vizuri wewe binafsi, na nafasi yako katika uhusiano wako.
- Kuweza kuanzisha na kuendesha uhusiano wenye afya.
- Namna ya kukuza na kuboresha mawasiliano ya kimapenzi.
- Umuhimu wa kusubiri kabla hujaanza uhusiano mpya.
- Jinsi ya kurekebisha uhusiano wenye ufa na kuuziba.
- Kitabu hiki kitakusaidia kukua kiakili, kisaikolojia na kihisia.
- Kitakupa uwezo wa kuyamiliki maisha yako.
- Kitakufanya utambue kuwa kuna maisha mengine baada ya uhusiano ulionao kufika tamati.
- Kutambua jinsi ya kurudiana na mpenzi ambaye mmeshaachana,mpenzi gani unaweza kurudiana naye, katika mazingira gani unaweza kufanya hivyo na ufanyaje ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kupatikana kwa kurudiana na mtu kiholela.

Ni kitabu ambacho kimekusanya mafundisho mengi kwa pamoja.

Namshukuru Mwenyezimungu kuniwezesha kuweza kukiandika pamoja na kukikamilisha.

**Marm-0653544133**
**Mariam Mbano**

# Anatuhusia Laura Pettie USTAHIMILIVU



**Na: Laura Pettie**

Ustahamilivu ni uvumilivu.
Ustahamilivu ni subira. Kiwango chako cha uvumilivu na subira katika mambo madogomadogo ya kibinadamu, yaliyo nje ya uwezo wa mtu mwingine au wako mwenyewe ni wa kiwango gani?

Umewahi kujitafakari?

- Kwa mfano, jambo lolote lisipoenda unavyotaka ndani ya sekunde tu mapigo ya moyo yanaenda kasi sana. Unajisikia kujihami. Unarusha maneno makali sana au hata kama utakaa kimya basi utateseka kimyakimya mwenyewe.

- Uwezo wa kujenga hoja unashuka na unatawaliwa na matusi, kejeli, vitisho, bezo au matumizi ya nguvu hata kwa mambo ya kuelekezana na kuelewana. Hapa sizungumzii wanaokuchokoza kwa matusi na kejeli. Yaani kitendo cha mtu kukusahihisha kistaarabu tu mihemko inakupanda ghafla. Hutataka kuielewa hoja yake utataka kumchakaza akujue we ni nani!

- Una hasira za haraka za mara kwa mara ambazo kila unapotulia na kufikiria ulichotenda unajiona ulikurupuka. Unakuwa mtu wa kufokea au kugombana na watu mara kwa mara.

- Unalazimisha sana mambo yawe unavyotaka wewe, yaende kwa haraka sana, huna subira ya kuona mwingine akifanya kitu kabla yako ndipo ufanye wewe. Unakuwa juujuu kila saa kama vile kuna kitu kitakupata hivi. Unaogopa kushindwa au kupitwa hata kwa vitu visivyohitaji ushindani.

- Huna utulivu wa nafsi hata kama kwa nje unaonekana ni mwenye utulivu. Jipime mwenyewe, pale unapokuwa nje ya macho ya watu unakuwa vipi kwenye mapokeo ya baadhi ya vitu?
Mfano kukwazika ovyo hata ukiwa unatafuta kitu mwenyewe, kumpiga mtoto au kumwita jina baya kwa sababu hakukusikia ulipomwita nk. Mtu anaeleza kitu usipokielewa sawasawa huna muda wa kuuliza uelewеshwe, unalipuka kumshambulia kwanza ili ujisikie nafuu.

- Uwezo wako wa kuwasikiliza watu wanaohitaji sana muda wako unashuka. Kwa mfano kumweleweshа mtu mzito kidogo kuelewa, kumsikiliza mwenye kigugumizi, kuongea na mtu mwenye usikivu hafifu, kusikiliza maswali ya udadisi ya mtoto na kuyajibu badala ya kuitikia tu chochote anachosema. Kusubiri mtu avuke barabara. Nk

- Unakuwa mwepesi kuhukumu hata kimoyomoyo na unapoteza hali ya kuwa na huruma ya dhati kwa sababu huna ustahamilivu wa kufikiria zaidi.

- Kitu kidogo unahisi hasira, jasho na nafsi kuhangaika.
Kuna namna nyingi za kupima viwango vyetu vya ustahamilivu kwenye mambo ya kibinadamu. 2022 panapo majaaliwa, ukawe mwaka wenye kutupa nafasi ya kujifunza kujielewa zaidi kitabia. Kujielewa kunakosaidia kuijenga vyema afya ya akili.
Ustahamilivu binafsi unapokuwa imara unajipunguzia mihemko ambayo ni rahisi pia kujizalishia magonjwa mbalimbali yatokanayo na msongo wa mawazo, sonona nk. Tunapojifunza ustahamilivu binafsi tunajifunza kuituliza akili na mwili. Tunajifunza kuiongoza mihemko na si mihemko kutuongoza kila mara.

Laura Pettie mwandishi wa vitabu Dira ya Moyo na Kiroba Cheusi. Ni moja ya waandishi mahiri wa kike hapa Tanzania. Wengi wanaomsoma wamempachika jina ***Fundi Mshona maneno.***

Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Uboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Ukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Uboresha Mtazamo na Umakini

# Ijue Taasisi ya THAYAKI

THAMANI YA KISWAHILI (**THAYAKI) ni taasisi isiyo ya kiserikali iliyojikita kwenye kukuza na kupigania Kiswahili katika kukipa thamani. Mkurugenzi wa taasisi hiyo Bwana Paulo Mzolo anatueleza kwa kifupi juu yake.**

Taasisi hii ilianza mwaka 2017 kama *program* na baadae nikaona ni vyema kuisajili kuwa NGO. Hivyo mwaka 2019 ikasajiliwa na kuwa NGO.
Wazo la kuanzisha taasisi hii lilitokana na mimi kama mwasisi kuona kwamba thamani ya lugha adhimu ya Kiswahili katika jamii ya Waswahili ni ndogo ukilinganisha na zile za kigeni kama Kiingereza na Kifaransa. Hii ndiyo ilinipelekea kuchukua hatua hii.
Lengo kuu la taasisi hii ni kukuza uelewa juu ya thamani ya lugha fasaha ya Kiswahli katika jamii kwa kuwezesha ushirikiano na muunganiko wa wadau na wataalamu wa lugha ya kiswahili. Pia kuhamasisha uibuaji na utambuaji vipaji vya uandishi, sanaa, tamaduni na michezo katika jamii.




**Paulo Isaya Mzolo**

Mpaka sasa tumefanya kazi katika mikoa ya Dar es salaam na Mwanza. Shughuli zetu tunaziendesha kwa ufadhili kulingana na matukio tunavyokua tumeyaandaa ila hatuna ufadhili rasmi wa moja kwa moja.

Katika haya yote, tunakumbana na changamoto nyingi tofauti tofauti kulingana na mazingira ya kazi tunavyokua tukifanya kama uchelewaji wa vibali mkiomba, uzito wa wadau na wahisani mkijipanga kuandaa matukio, mwitikio wa wataalamu katika kuwapa Ushirikiano na changamoto za kiuchumi katika kuinua shirika na watendaji wake

Wito wangu kwa watanzania ni kupenda lugha yetu na kuipa thamani ya kwanza katika kila nyanja, tasnia na hafla zetu ili kuonyesha jinsi gani tunajali cha kwetu na tunakitumia bila uwoga!

# Je; kusoma ni muhimu katika maisha yetu? - 4



**Na: Mwandishi wetu**

Katika toleo lililopita tuliangazia faida za kusoma vitabu. Andiko letu linaendelea katika toleo hili.

Faida za usomaji vitabu

**3. Ujuzi**
Kila kitu unachosoma kitakijaza kichwa chako na mambo mapya, na huwezi jua kipi kitakujia mkononi mwako. Ukiwa na ujuzi zaidi ndivyo utavyoweza kupambana na changamoto zinazokukabili.

Kwa nyongeza, hebu fikiria: umeshawahi kujikuta katika hali mbaya, kumbuka kwamba umepoteza kazi, umepoteza mali, na kila kitu hata afya yako - lakini ujuzi hauwezi kuondoka.

**4. Kuongeza msamiati**


Hii inaendana na dondoo namba 3:

Unavyosoma zaidi, ndivyo unavyokutana na msamiati mwingi mpya ambao unakuja kuwa maneno yako ya kutumia kila Siku.

Kuwa mwongeaji mahiri na mfafanuzi mzuri wa jambo ni kitu muhimu sana katika taaluma yoyote ile, na kujijua kuwa unaweza kuongea kwenye majukwaa makubwa kwa kujiamini yaweza ukuongezea hali ya kujithamini. Yaweza kuwa hata msaada kwenye tasnia yako. Kwa wale wasomaji wazuri, waongeaji wazuri na wenye ujuzi katika mada anuai huwa wanapata wanapata nafasi za juu au kupanda vyeo haraka (na Mara nyingi) zaidi ya wale wenye uhaba katika msamiati, mapungufu katika ufahamu wa kifasihi, kujua mafanikio ya kisayansi duniani na matukio ya kiulimwengu.

Kusoma vitabu pia ni muhimu kwa kujifunza lugha mpya, kama si wazungumzaji wa asili wa lugha hiyo twapata mfiduo kwa maneno yaliyotumiwa katika muktadha, ambayo yatafurahisha katika mazungumzo na maandiko yao ya kila siku.

***Itaendelea toleo lijalo***




## Makala ya Kijasusi

## VIRGINIA HALL, MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU— 01

Na Mwandishi wetu

**Virginia Hall ni mmoja kati ya majasusi muhimu sana wa Marekani ambaye hakuwahi kusikika.**

Simulizi yake inapatikana kwenye bango la onesho ndani ya Makumbusho ya CIA yaliyopo kwenye Makao makuu ya CIA huko Langley, Va.— lakini haikuwa kwa ajili ya kila mtu. "Alikuwa ni mwanamke mwenye kujipamba sana wakati wa Vita ya Pili ya Dunia," anasema Janelle Neises, mkurugenzi msaidizi, anayesimamia makumbusho hayo.

Kwanini watu zaidi hawajasikia kuhusu Hall? Nukuu kutoka kwenye maandishi yake ya kijasusi inatoa maelezo juu ya hili: "Marafiki zangu wengi waliuawa kwa kuwa walikuwa wanaongea sana."

Lakini sasa – zaidi ya miaka 70 baada ya mlipuko wa vita huko Ufaransa, na baada ya takribani miaka 40 baada ya kifo chake – Virginia Hall anapata nafasi. Vitabu vitatu vimechapwa. Filamu mbili zinatengenezwa. Mwandishi wa vitabu wa Uingereza Sonia Purnell ameandika moja ya vitabu hivyo, Mwanamke Asiye na Umuhimu, na amemkejeli kwenye kichwa cha wasifu wake "Pamoja na mengi ya maisha yake, maisha yake ya awali, alikataliwa na kudharauliwa " ameandika Purnell. "daima amekuwa akifukuzwa ama kupuuzwa kama mtu ambaye si muhimu au hana umuhimu." Hall alizaliwa kwenye familia ya kitajiri ya Baltimore mwaka



1906, malezi yake yalimfanya aolewe na yule ampendae. Lakini alitaka zaidi matukio ya hatari. Alipenda kujiita "asiyebadilika na wa kuogofya." Alipenda kuwinda. Mara moja aliwahi kwenda shule akiwa na kembe lililotengenezwa kwa nyoka walio hai.

**Elimu Ufaransa**

Kwa kifupi, Hall amesoma katika chuo cha Radcliffe na Barnard. Halafu akaenda kusoma huko Paris na kujikuta akiipenda Ufaransa. Purnell anasema, Hall aliamua kuwa mwanadiplomasia.

"Alitaka kuwa balozi. Aliwekwa pembeni na idara za kiserikali. Aliomba mara nyingi," anasema Purnell.

Hall alifanya kazi ya ukarani wa ardhi katika ubalozi mdogo wa Marekani nchini Uturuki. Lakini wakati akiwinda ndege, alijifyatulia risasi mguuni kwa bahati mbaya. Akapata donda ndugu, hivyo mguu wake ukakatwa kuanzia chini ya goti.

Kupona kwake kulichukua muda mrefu na kupitia maumivu makali, hasa alipokuwa akijifunza kutumia mguu wa bandia uliotengenezwa kwa mbao. Huo ulikuwa ni wakati wa mabadiliko, anasema Craig Gralley, afisa mstahafu wa CIA ambaye aliandika kitabu chake kumhusu mwanamke huyo – alichokipa jina Hall of Mirrors. "Alipewa nafasi nyingine katika maisha, na hakupenda kuipoteza. Na jeraha lake, kiukweli, lilimuimarisha au kuamsha uthabiti wake hivyo akawa mwenye kufanya mambo makubwa zaidi, ," Craig Gralley anasema.

**Makala hii imetafsiriwa kutoka kwenye mtandao. Itaendelea toleo lijalo**

RIWAYA



Richard Mwambe

# MPIGA MBIO — 04

**Vazi alilovaa liliuelezea mwili wake. Kenneth alimtazama biti huyo wakati akielekea upande wake, macho yao yakagongana….**

Ikunda alijikuta anaingiwa ganzi mwilini, moyo wake ukadunda kwa kishindo, miguu ikasita kutembea. Akasimama kwa sekunde kadhaa akijifanya kama anafikiri jambo, kisha akaendelea na safari yake.
"Samahani dada!" akasikia sauti kutoka nyuma yake ikiita kwa utulivu. Akasimama na kumtazama huyo amwitae.

"Bila samahani…" Ikunda akajibu.
"Nahitaji msaada japokuwa nitakuwa navunja utaratibu…"
"Sema!" Ikunda akamwambia huku akiwa haamini kama imewezekana. "Ninahitaji kudipoziti pesa, lakini kwa foleni hii nahisi kushindwa, unaweza kunisaidia?" Kenneth akamwambia Ikunda kwa toni ya sauti ambayo huwezi kukataa ombi. Kenneth alijua kuomba.
"Mh!" Ikunda akaguna huku akiangalia saa yake ndogo ya mkononi, "Nitajaribu!"
"Usijaribu, fanya kabisa…" Kenneth akabembeleza.
"Sawa, andika na namba yako ili nikikamilisha nikutafute…" Ikunda akamwambia Kenneth. Naye akafanya hivyo. Asilimia kubwa ya watu waliokuwa eneo hilo waliwatazama. Sijui waliwatazama kwa lipi. Baada ya zoezi hilo Kenneth akaondoka na Ikunda akaendelea na kazi huku akitabasamu usoni. Siku hii ilikuwa kama ndiyo kazaliwa vile. Ikunda akatoka nje ya ule mlango mkubwa japo tu amsindikize kwa macho. Alipofika nje, hakumwona Kenneth. Akaangaza macho huku na kule, hayupo.
*Mtu au mzuka?* Akajiuliza. Alipogeuka kurudi, akachomoa simu janja yake na kupiga picha japo wayo wa kiatu cha mwanaume yule. Ikunda alianguka penzini. Penzi lisilokuwepo! Kwa kupokea kazi ile alijua tu atamnasa kijana huyo. Kijana jamali wa umbo, sura na kadhalika.
Mara aliporudi ndani, jambo la kwanza lilikuwa ni kuifungua ile bahasha ili kujua mwanaume huyo anaweka kiasi gani cha fedha. Maana bahasha ile ilikuwa nyepesi kama imewekwa jani la kisamvu. Alipoifungua, macho yalimtoka pima. Akajilaumu kwa nini alikubali bila kujua kilichomo ndani. Hundi ya shilingi za Kitanzania milioni kumi na tatu nukta sita ililala kiganjani pake.
*Angedipoziti mwenyewe!* Akawaza. Lakini akapiga moyo konde na kuzunguka upande wa pili mpaka kwa shogaye, Prisca.
Prisca hakuwa na watu muda huo alikwishaweka *'temporary closed'* kwenye kidirisha chake.
"Shoga msaada!" akamwambia huku akimpatia ile hundi. Prisca akaipokea na kuisoma, "huyu jamaa sijui pesa anatoaga wapi!"
"Kwanini?" Ikunda akadakiza swali.
"Kila akija hapa ni hundi au keshi ya mamilioni… mi ningempata mwanaume kama huyu ningemfaidi kwa jinsi zote…" Aisha akaongea kwa bashasha. Ikunda akabaki kimya akijaribu kuyamumunya maneno ya shogaye. "Shoga we hii hundi kakukabidhi wapi? Sasa na hizi saini hapa ataweka nani? Au we mwenyewe?" Prisca akamuuliza Ikunda.
"Panahitajika saini tena?" akauliza.
"Ee! Shoga ushamnasa nini hebu nijuze mwanamke mwenzangu…"
Prisca akaongea kwa ubembe huku akichakata baobonye la kompyuta yake. Ikunda akamkazia Jicho shogaye, "Mi siyo wa hivyo… nimemsaidia tu!"
Ni kweli, Ikunda katika makuzi yake hakuwa na tabia ya kurukaruka na wanaume. Mpaka umri huo alionao wa miaka ishirini na minane alikuwa bikra, kigoli, mbeja. Ijapokuwa umri ulizidi kwenda, hata yeye alitamani mume, alitamani mtoto lakini bado alikuwa na woga kidogo katika swala zima la ndoa na tendo lake. Aliona ndoa nyingi zikivunjika, wanawake wengi wakipata ulemavu na hata majeraha ya kihisia, kisa ndoa. Zaidi ya hapo tangu akiwa anakua alisikia rafiki zake, alisoma kwenye riwaya za mapenzi kuwa kwenye tendo hilo wanawake hulia sana, aliogopa. Lakini sasa alijikuta hoi, alimpenda mwanaume. Macho yalimwona huyo kijana, moyo ukamchagua, lakini bado mdomo ulikuwa mzito kusema 'nakupenda'. Alikumbuka siku moja akiwa kwao, na ukubwa huohuo alienda kumtembelea rafikiye Siyawezi. ***Itaendelea toleo lijalo***

**PITIO LA VITABU**

# ADILI NA NDUGUZE—02



Na: Maundu Mwingizi
(Mwanabalagha),
Mtu wa Tabora.

**Shaaban Robert anatujulisha kwamba, kama uzuri wote wa peponi wamejaaliwa Malaika, basi karibu uzuri wote wa duniani alijaaliwa msichana huyo.**


Mbali ya uso wake kutukuka kwa uzuri huo, pia tunaambiwa kuwa alivalia libasi nzuri na za thamani kubwa, zenye rangi nzuri na za almaria bora kabisa. Msichana huyo aliitwa Mwelekevu.

Sasa baada ya Adili kufika chomboni, alishangiliwa na kila mmoja. Na kwa moyo uleule wa upendo, akagawanya mali yake mafungu sawa kwa nduguze, mabaharia na nahodha bila kujali kuwa mali ile hawakuipata kwa shirika. Alichozingatia yeye ni ukweli kwamba, siku zote mkulima alikuwa mmoja ila walaji ni wengi. Lakini tazama ufidhuli wa ndugu zake, badala ya kushukuru na kutosheka kwa walichogawiwa, wao walisalitika na mapenzi kwa uzuri wa Bi Mwelekevu. Wakaanza kumzengea huku kila mmoja akitaka kumchukua yeye. Baada ya kuona Adili amewagomea kumchukua, wakatoa rai kwamba basi wamtumie shirika. Baada ya Adili kukataa pia shauri lao hilo, ndipo walimvizia akiwa usingizini wakambeba hangahanga na kumtosa baharini ili tu wamchuke msichana yule. Kuona hivyo, msichana yule akaona ni akheri kufa kuliko kuguswa na madhalimu wale, naye akajitosa baharini. Sasa wakawa wamekosa mwana na maji ya moto.

Mara baada ya Adili kuzama baharini na kuibuka, akiwa anatapatapa kujaribu kujiokoa, ghafla alitokea ndege mwenye umbile la kutisha, akamwopoa Adili majini na kupaa naye angani. Ndege yule alipaa juu kwa kasi na kwa umbali mrefu mpaka Adili akapoteza fahamu. Kuja kuzinduka akajikuta yu-ndani ya jumba la kifakhari huku mbele ya macho yake akiona wasichana warembo wakimhudumia bi mkubwa mmoja aliyejipambanua kama malkia wa himaya ile. Mara, ndege yule aliyemwopoa alijigeuza na kuwa msichana mrembo mno. Unajua msichana mwenyewe alikuwa nani basi? Alikuwa yule aliyeokolewa na Adili akiwa Tandu aliyetaka kuuliwa na nyoka - jina lake aliitwa Huria binti Kisasi. Huria alimsogelea mama yake, malkia Mjeledi, na kumsimulia kisa cha Adili kumwokoa siku ile. Kwa furaha malkia alimpa mkono Adili na kumshukuru kwa kumwokoa bintiye.




Huria binti Kisasi alimsimulia Adili kwa matayasari juu ya kisa cha yule nyoka aliyekusudia kumtenda vibaya siku ile. Nyoka yule akiitwa Hunde, alikuwa ni jini mwenye cheo cha Waziri wa Ngazi katika utawala wa mfalme Kisasi, ambaye ndiye baba yake Huria. Hunde alikuwa na sura mbaya kupita majini wote. Siku moja matembezini, Hunde alikutana na Huria akavutiwa naye. Katika suala la wanawake kutamaniwa wakati mwingine na watu wa ovyo na kuanza kusumbuliwa, Shaaban Robert anasema, Wanawake hukutana na mikasa mingi mibaya duniani. Mioyo yao huelemewa na haja zisizokubalika; masikio yao hutiwa uziwi na maombi ya haraka;



**SHABAN ROBERT**

na daima miili yao ni mawindo ya jeuri. Hunde akaenda kumposa Huria kwa mfalme Kisasi. Mfalme akamkatalia katakata.

***Itaendelea toleo lijalo***

# Tangazo

**Soma kitabu kikukomboe kifikra na kimtazamo**

## PATA NAKALA ZA VITABU VYA RIWAYA KATIKA SEHEMU ZIFUATAZO

### DAR ES SALAAM:

- Duka la Kona ya Riwaya—Kinondoni

  **Tel: 0655 428 085** –Zamira

- Posta Mpya Karibu na mzunguko wa Askari

  **Tel: 0755 454 152** George

### MOROGORO:

- Kituo cha Daladala, Bima Samaki Samaki

  **Tel: 0748 623 743**

### ARUSHA:

- Wakala nje ya duka la Kimahama
  Tel: 0757 690 302

### MBEYA:

- Duka la vitabu FANANI na HADHIRA
  Tel: 046 840 840

### IRINGA:

- Fika Stationary kubwa ya LUTENGANO


**Simu: +255766974865**
**Insta: jamvi la Simulizi**
**Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

**Ngurumo ya Mwandishi**
**S.L.P 1039**
**Iringa**
**Whatsapp: +255734550514**

**Msanifu wa Jalada: Nnepei Graphics — 0624310506**


## MTUNZI WETU: GASPER MPOMA



Ninaitwa Gasper Mpoma, almaarufu kwa jina la kiandishi GASPER WA MASTORY.

Ni mzaliwa wa Iringa Wilaya ya Kilolo, mnamo mwaka 1998, Agosti tarehe 4. Sabasaba ilikuwa shule yangu ya msingi, na Kleruu ndiyo Sekondari niliyosoma O level na baadae Madibila nikajiunga A level. Mimi ni muhitimu wa Shahada ya kwanza ya Sanaa katika Mahusiano ya Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Tangu nikiwa mdogo nilipenda kusoma simulizi hasa kwenye magazeti na majarida mbalimbali.

Nilianza kuandika simulizi nikiwa darasa la saba, 2011. nilipokuwa kidato cha nne ndipo niliandika kwa umakini zaidi.

Kuna changamoto nyingi sana nimepitia katika safari hii ya uandishi ikiwamo uthamini wa kazi kutoka kwa mashabiki wangu. Wapo waliozichukulia kawaida na kusahau jasho na bidii niliyoweka. Pia wapo waliozidukua mtandaoni na kunirudisha nyuma, si mimi tu hata kazi za wengine. Na jambo lingiine ni kukosekana kwa ushirikiano na waandishi wengine hasa wanaomiliki ma*group* makubwa ya *facebook*.

Mimi ninaandika simulizi za mapenzi na mikasa ya maisha.

Kama kuna kitu kinanivutia basi ni wanawake waliojikita kufanya kweli kwenye tasnia hii. Siwezi wataja wote, lakini wapo wenye uwezo mkubwa sana ila tu hawajiamini. Napenda kuwaambia wasiogope, wasisite bali watumie au waanze na walichonacho, watafika mbali.

Mpaka sasa nimeandika riwaya nne; KIBUTI, UGENINI, MBONA HAJIONGEZI na NILIKUTANA NA JINI CHUONI.

Zote zinapatikana kwenye kurasa yangu ya facebook inayoitwa Simulizi Tamu za Gasper.

Riwaya, NILIKUTANA NA JINI CHUONI, inapatikana kwenye gazeti la JIJI na App ya Mpaper.

**Nipate Whatsapp: 0656322828**